

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA

SHULE YA SEKONDARI MSOWERO
S.L.P 6097,
MOROGORO
15/12/2019

Kumb.Na:MSOSS/ADM/F.1/2020

.....
.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MSOWERO
WILAYA YA KILOSA, MOROGORO
MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI

Ninayofuraha kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga na Elimu ya sekondari (kidato cha kwanza) katika shule hii. Shule ya sekondari Msowero ipo katika kijiji cha Msowero, Kata ya Msowero, Tarafa ya Magole, umbali wa takribani km 42 kutoka makao makuu ya Wilaya ya Kilosa, Mkoani Morogoro.

Muhula wa masomo utanza siku ya jumatatu tarehe 11/1/2021 saa 1:30 Asubuhi. Hivyo wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti siku hiyo. Kwa sababu yoyote ile, hakuna mwanafunzi atakaepokelewa baada ya kipindi cha siku saba kuanzia tarehe 18/1/2021 na hatua zingine za kisheria zitafuata kwa kumchelewesha mwanafunzi .

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Mwanafunzi unahitajika kuwa na vitu vifuatavyo ili upokelewe shuleni-:

2.1 SARE ZA SHULE

(a)MVULANA

- i) Suruali mbili za rangi ya Khaki zenye mifuko mitatu (isiyo ya kubandika). Ziwe za heshima, siyo za kubana au "modo". Vipimo vya chini kwenye mguu isiwe zaidi ya inchi 15; vinginevyo hazitakubalika.
- (ii) Mashati mawili meupe ya tetron (Tomato) yenye mikono mifupi.
- (iii) T-shirt 1 yenye nembo ya shule - Inapatikana shuleni kwa sh.12,000/=
- (iv) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na vinavyofungwa kwa kwamba
- v) Tai ndefu iliyoshonwa kwa kitambaa cha rangi ya suruali ya shule.
- (vi) Soksi jozi mbili za rangi nyeupe.
- (vii) Sweta rangi ya buluu

(b)MSICHANA

- (i) Sketi mbili za rangi ya Khaki. Mashono aina ya "Rinda box" ziwe ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu.
- (ii) Mashati mawili meupe ya tetron (Tomato) yenye mikono mifupi/juba

- (iii) T-shirt 1 yenye nembo ya shule-Inapatikana shuleni kwa sh.12,000/=
- (iv) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na vinavyofungwa kwa kamba.
- (v) Tai ndefu iliyoshonwa kwa kitambaa cha rangi ya suruali/sketi ya shule.
- (vi) Soksi jozi mbili za rangi nyeupe.
- (vii) Sweta rangi ya buluu

2.2 VIFAA VYA DARASANI

(c) WAVULANA NA WASICHANA:

- (i) Madaftari makubwa (counter book q2 kumi 10.
- (ii) Kalamu ya bluu/nyeusi
- (iii) Mkebe (Mathematical set)
- (iv) Kamusi ya Kiingereza na Kiswahili
- (v) Rimu nyeupe isiyo na mistari.
- (vi) File folder moja(1)
- (vii) Begi la kubebea madaftari.

2.3 VIFAA VYA USAFI

(d) WAVULANA NA WASICHANA

- (i) Jembe lenye mpini
- (ii) Fyekeo/Kwanja (wasichana)
- (iii) Panga(wavulana)
- (iv) Ndoo ndogo 1.
- (v) Ufagio wa chelewa

2.4. MAVAZI YA MICHEZO:

Raba, socks, jezi rangi ya manjano(kwa wasichana)na rangi nyekundu (kwa wavulana) Saa ya mkononi.

NB:Vifaa vyote hivi ni lazima na vitahakikiwa siku ya kuripoti shuleni.Atakayepungukiwa vifaa hata kimoja hatapokelewa.

3.0. HITIMISHO

Nakupongeza tena kwa kuchaguliwa kwako nikiamini kuwa utatumia nafasi hii uliyopata kusoma kwa bidii na kuwa mfano wa kuigwa kwa tabia na mwenendo mzuri ili hatimaye ufikie malengo yako kwa manufaa yako na Taifa kwa ujumla.

Mwisho,Nimekuwekea viambatisho vifuatavyo;-

- Kiambatisho Na.I- Sheria na taratibu muhimu za shule.Tafadhali zisome na kuzielewa ili ziwe dira ya maisha yako ya uanafunzi hapa shuleni.
- Kiambatisho Na.II- Fomu ya usajili na Tamko la utii wa sheria.Fomu hii uijaze wewe mwenyewe pamoja na mzazi/mlezi wako kwa usahihi.
- Kiambatisho Na.III- Medical examination form.Unatakiwa kupeleka kwa daktari wa kituo cha tiba kinachotambuliwa na serikali ili akupime na kukujazia fomu hii.

NB. Viambatisho na. II na III viwasilishwe kwa mkuu wa shule siku utakaporipoti shuleni vikiwa vimejazwa na wahusika kwa usahihi.

Nakutakia maandalizi mema na karibu sana shule ya sekondari Msowero!.

.....
JOSEPHINE MICHAEL NAKEI
MKUU WA SHULE

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA
SHULE YA SEKONDARI MSOWERO
S.L.P 6097, MOROGORO**

Kiambata Na. I

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa Mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria ya Na 10 ya 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya RAIS TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu.

Hivyo mwanafunzi unapaswa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
3. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(evening preparation).
4. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
6. Kuzingatia usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule .
7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa .
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
9. Kutunza mali za umma.

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kuberi, ugoro, sigara nk
5. Kupiga au kupigana
6. Kuharibu kwa makusudi mali za umma
7. Kudharau bendera ya taifa
8. Kuwa mjamzito au kusababisha mimba
9. Kuo au kuolewa
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule, jamii na watu wengine.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kuwa na simu ya mkononi ukiwa shuleni

Nakutakia utekelezaji mwema

MKUU WA SHULE

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA
SHULE YA SEKONDARI MSOWERO
S.L.P 6097, MOROGORO**

Kiambata Na. II

FOMU YA USAJILI NA TAMKO LA UTII WA SHERIA

SEHEMU A: Ijazwe na Mwanafunzi

Jina la mwanafunzi: _____ jinsi (ME/KE) _____

Tarehe ya kuzaliwa _____ mahali pa kuzaliwa _____

Dini: _____ Kabila: _____

Jina la Mzazi/Mlezi _____ kazi yake _____

Namba yake ya simu _____ anuani _____

Tamko: Nakiri kwamba nimesoma kwa makini sheria za shule na kuzielewa.

Nimekubali na _____ nina ahidi kuzitii kwa manufaa yangu, shule, na umma
kwa ujumla.

Saini ya mwanafunzi _____ Tarehe _____

SEHEMU B: Ijazwe na Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi

Mimi _____ nakiri kwamba nimesoma kwa makini Sheria
za Shule na maelekezo yote kama yalivyoandikwa katika barua ya tarehe 15/12/2020 na
kuzielewa vizuri.

Nimekubali na ninaahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule kuhakikisha kuwa mtoto
wangu (Jina) _____ anafuata sheria na
kanuni za shule na kusoma kwa bidi.

Pia nitahakikisha mtoto wangu anapata mahitaji yote muhimu ya shule kwa wakati. Aidha
kama Mzazi/Mlezi ninatambua kuwa Elimu ni haki ya msingi ya mtoto, hivyo ni wajibu wangu
kuhakikisha mtoto wangu anahudhuria darasani (shuleni) kila siku na kupata elimu kwa
manufaa yake na kwa taifa kwa ujumla.

Saini ya mzazi/mlezi _____ Tarehe _____

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KILOSA DISTRICT COUNCIL
MSOWERO SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 6097, MOROGORO**

Kiambata Na. III

TO THE MEDICAL OFFICER,

Kindly examine the below named student and record the results in this form

STUDENT' NAMES: _____ SEX _____ AGE _____

A. MEDICAL HISTORY:

TEST FOR	YES	NO
Tuberculosis		
Asthma		
Heart disease		
Jaundice		
Peptic ulcers		
Epilepsy		
Diabetes mellitus		
Kidney problem		
Anemia		
Neurosis		

B: PHYSICAL EXAMINATION

Respiratory system _____

Cardiovascular system _____

Gastrointestinal system _____

Urinary system _____

Reproductive system _____

Eye R _____

L _____

E.N.T _____

C. INVESTIGATION:

1. Blood HB _____

WBC _____

ESR _____

VDRL Test _____

2. Urine - Pregnancy _____

- Sed _____

3. Stool _____

I have examined the above student and considered that he/she is physical and mentally fit/unfit for further studies.

Medical officer's names _____

Signature _____ designation _____

Station _____ Date _____ Official stamp _____